KISWAHILI KARATASI YA 3

KCSE 2025

MWONGOZO KCSE 2025

1. a) i) ni maneno ya Asna akiambia mamake Sara walkiwa chumbani mwa Asna mjini. Hii ni baada ya Sara kustaajabu kwa nini hakutaka kuihi mashambani na akaiari kuishi mjini. Akamjibu kuwa maisha ni kujaribu
   ii) taswira hisi- mahuluki kuhisi maisha ya taabu.
   Taswira mguso – kushikilia chochote
   iii)
   i. Asna anatambulisha sifa za Sara kuwa ni mtamaduni kwa kumshawihi kuwa msichana aliyebaleghe lazima kuoleka
   ii. Anaonyesha mabadiliko yaliyoko kati ya maisha ya kisasa nay a zamani
   iii. Anaonyesha changamoto wanazopitia vijana katika harakati zao za kutafuta ajira
   iv. Kiungo muhimu kati ya Neema na Sara katika harakati za kutafuta matibabu
   v. Anatambulisha msingi wa wivu alionao kwa Bunju
   vi. Anaendeleza ploti kwa kumkubalia Sara kukaa naye ili keshoye aende kutibiwa
   vii. Kielelezo cha wasichana wenye bidi masomoni, alifuzu chuo kikuu
   viii. Mfano bora wa wasichana wenye ukengeushi, hauko tayari kuoleka
   ix. Anatumika kuonyesha umuhimu wa kuwa na msimamo dhabiti, licha ya vishawishi vya mamake hakubali kuoleka
   x. Anaonyesha suala la utabaka mjini, anaishi servant quarters huku mwenyeji wake akiishi kwa kasri.
   b)
   i. Yona anakumbuka jinsi alivyokuwa mwerevu chuoni- anakuza maudhui ya elimu
   ii. Yona anakumbuka alivyoshawishika na wenzake kuanza ulevi – maudhui ya ulevi
   iii. Dina anakumbuka namna Sara na Yona walivyosenyenywa kwa kukosa mtoto – maudhui ya umbeya
   iv. Dina anakumbuka vishawishi kwa Yona kuoa mke mwingine- maudhui ya ubabedume
   v. Yona kutishia kumtalaki Sara- maudhui ya ndoa
   vi. Sara kukumbuka kuachishwa kusoma ili kuoleka- uatamaduni
   vii. Neema anakumbuka jinsi baba yao alivyowatelekeza – malezi
   viii. Dina kuoleza jinsi Yona alivyokuwa akimpiga Sara - ukatili
2. a) maneno ya mwandishi akimrejelea Mwangasha (uk 13) akiwa kanisani baada ya kufurushwa kutoka katika makaazi yao na nyumba zao kuchomewa. Anashanga namna atakavyowabadilisha fikra za watu wa jamii yake dhidi ya ukatili wa aina hii ya kufurushwa kutoka kwa makaazi.
   b) kutuliza/kuhimza/kuliwaza/kujishajiisha- anajipa tumaini kuwa mchango wake mdogo utabadilisha mtazamo wa watu wake licha ya kutendewa maovu.
   c) i) msemo – fikra zilienda mrama/piga mbizi – kuonyesha hali ya taharuki iliyomkumba
   ii) taswira – kupigia mbizi – kusistiza jitihada zake za kutafuta ukombozi

www.kala.co.ke

iii) Istiari/jazanda – kulipigia mbizi tatizo- uamuzi wake wa kutafuta suluhu

d) Mhusika ni Mangwasha

i. Anaendeleza ploti- kiungo/mwendakati kati ya Ofisi Ya chifu na Lonare
ii. Anatambulisha sifa za Mrima kuwa mwepesi wa kushawishika
iii. Anaonyesha mchango wa kina mama katika ukombozi- anashirikiana na Lonare
iv. Kielelezo cha wanawake waliotayari kujikomboa kutoka kwa tamamaduni- kumtafuta Mrima licha ya Mbungulu kumkataza
v. Anatumika kufichua biashara haramu za Sihaba – madanguro
vi. Anatumika kuonyesha kuwa Mrima ni msherati- barua kutoka kwa mpenzi
vii. Kiungo muhimu cha ukombozi- Lonare alipatikana kwake na kumpeleka sipitali
viii. Mfano bora wa jitihihada za kuwakomboa vijana- kuanzisha shirika.
ix. Anaonyesha ghadhabu na majuto ya chifu Mshabaha- kumwendea ili apewe msaada
x. Anadhihirisha kuwa ukombozi hutokokana na kujitolea mhanga- kufilisika/kufutwa kazi
xi. Mfano wa wanawake walio radhi kutunza ndoa zao licha ya changamogto kutoka kwa waume zao – Mrima kuwa mlevi

3. a)

i. Swali balagha- balaa gani hii?
ii. Msemo – kugungua ukurasa mpya
iii. Takriri – ukurasa
iv. Kinaya- kusaka kazi zisizopatikana
v. Uhuishi- hela zilizowakimbia
vi. Jazanda – ukurasa ambao kila mtu angetaka kuwa nao

b)

i. Kunyakua vipande vya ardhi- Nanzia/Sihaba
ii. Kutolipa ushuru forodhani- Sagilu
iii. Kuagiza maziwa ya vijasumu nakuuzia raia – Sagilu
iv. Wizi wa kura – Lesulia
v. Biashara haramu ya madanguro – Sihaba
vi. Uuzaji wa madawa ya kulevya – Ngoswe
vii. Usherati – Sagilu kunyakua bibi za watu wengine
viii. Kuhonga/kushawishi wapiga kura – kuchaguliwa mara mbili kwa njia isiyo halali
ix. Kesi haramu kortini na kuhukumu wapinzani- Mafamba
x. Biashara haramu kwa wahanga wa mkasa – Mbwashu
xi. Wakule kupewa ajira huku Wakule wakitengwa
xii. Magari ya wapinzani kuzuiliwa ili ya vibaraka kuwachiliwa – Lonare
xiii. Pombe haramu kupigwa marufuku huku vibaraka wakiendelea kuuza.
xiv. Biashara haramu ya ukataji miti.
xv. Uidhinishaji wa ujenzi wa mijengo kwa njia isio halali- Mashauri

4. a)

i) maneno ya mwandishi. Akirejelea mazungumzo ya mjombake Adan akimfokea Adan. Wakiwa nyumbani kwa mojambake. Hii ni baada ya mjombake kusikia

www.kala.co.ke

uamuzi wa Adan kumruhusu Fadhumo kuendelea na masomo. Alikuwa ameghadhabika kwa sababu alihofu ya kuwa masomo ya Fadhumo yatamfanya amdhibiti Adan katika ndoa.

ii) i. Uradidi – kuonyesha taharuki. Kufoka kwa mjomba kulimfanya Adan kuchanganyikiwa kufanya uamuzi wa kumsikiza mjomba au kushadidia uamuzi wa kumruhusi Fadhumo kusoma

ii. Taswira – kuna taswira hisi ya kuonyesha hisia za mjomba kukasirikia uamuzi wa Adan kuruhusu Fadhumo kuondelea na masomo. Taswira hisi kwa Adan kumpenda Fadhumo na kuwa tayari kumruhusu kuendelea na masomo.

iii) Anayerejelewa na mjombake Adan

i. Anaonyesha uhafidhina- haamini kuwa mke anaweza kuendelea na masomo katika ndoa
ii. Anachimuza maudhui ya ubabedume kuwa mke aliyesoma hawezi kuheshimu mumewe
iii. Anasaidia kutambulisha uamuzi wa Adan, lazima atii ahadi kwa Fadhumo
iv. Anasaidia kujenga taharuki kati ya uamuzi wa Adan
v. Kufoka kwake kunasisistiza sifa ya Adan kuwa na msimamo dhabiti
vi. Anaonyesha changamoto wanazopitia wanawake wenye jitihada za kusoma

b) Umuhimu wa barua

i. Kuonyesha kuwa Suluhu alinyakua shamba la kina Abigael
ii. Kuonyesha kuwa Suluhu ndiye aliyeua mamake Abigael
iii. Kuthibitisha njia zisizo halali katika kutafuta kura
iv. Kuonyesha umaskini walionao Suluhu kabla ya kuwa mbunge
v. Kuonyesha kazi ya uchomaji makaa aliyokuwa akifanya Suluhu
vi. Kuthibitisha ukware wa Suluhu kuwa alikuwa na wasichana wengine chuoni
vii. ni ushahidi kuwa Suluhu anatelekeza familia yake.
viii. Kujuza kuwa wanawe wawili wanaumia kwa kukosa malezi bora
ix. Alimtunga binti mmoja mimba chuoni na kumwacha bila tumaini
x. Inafichua kuwa alikuwa akifuja pesa za wananchi kwa kuwalipa wasichana wa vyuo vikuu kukula uroda
xi. Kufichua kuwa alishindwa kumlipa Ngoma pesa alizokopa kufanya kampeni
xii. Kukumbusha kuwa awali alikuwa akimsaidia mama mkwe
xiii. Kwamba mkewe anawazia mauko/kujitia kitanzi
xiv. Kwamba amkome Abigael kwa sababu anaweza kumwambukiza nakama
xv. Kwamba yeye ndio chanzo cha mauko ya bibi yake

5. A) mandhari ya **Coco Beach**

i. Kuonyesha maudhui ya tamaa ya mapenzi ya Tumaini
ii. Maudhui ya uabudu shetani na Romea
iii. Maudhui ya anasa ya Tumaini na Romeo
iv. Maudhui ya ahadi za uongo kutoka kwa Romeo kwa Tumaini

www.kala.co.ke

v. Maudhui ya utajiri, gari la Q5.
vi. Maudhui ya ukengeushi, Romeo kuvaa kaptula
vii. Maudhui ya pupa ya Tumaini, kujiingiza katika mapenzi bila tahadhari.

Mandhari ya mtaa wa Kariokoo

viii. Ukarimu wa Jenifa
ix. Ukosefu wa ajira
x. Umaskini wa Jenifa
xi. Utajiri wa Nina

B) **Wahusika**

i. Nina kuwa mkarimu kwa Tumaini
ii. Nina kuwa na mapenzi ya dhati kwa Tumaini
iii. Jenifa kuwa mwenye bidii kazini
iv. Tumaini kuwa na tumaini la kupata ajira
v. Tumaini kuwa na pupa
vi. Tumaini kuwa jasiri
vii. Romeo kuwa laghai
viii. Romeo kuamini ushirikina
ix. Romeo kuwa mkengeushi
x. Romeo kuwa mpenda anasa na starehe

6. a. **Ujumbe**

i. Rafiki mzuri wa kuonekana mchana na usiki anakutenga sio rafiki
ii. Rafiki wa kutaka umsaidie nawe ukiwa na shida hakusaidii sio rafiki
iii. Rafiki mzuri hawezi kukusengenya
iv. Rafiki wa kumkaribisha kwa mlo kisha akiondoka anaanza kulaani huyo si rafiki
v. Rafiki wa kujifanya kuja kukuauni kisha aanze kukutangaza sio rafiki mwema
vi. Rafiki wa kumfichulia siri na mkiwa kwa safari anakudhuru sio rafiki

b. **Mitindo**

i. Mdokezo – ukiwa naye rafiki…
ii. Utohozi- tani
iii. Taswira – mkicheka vinywani
iv. Tabaini – si mchana wala usiku
v. Tanakuzi – mchana wala usiku
vi. Balagha – unasema una nini?

c. Uhuru wa kishairi

i. Vikale – maningani-machoni
ii. Inkisari – umualikaye-unayemwalika, aso – asiye
iii. Mazida – manyamani
iv. Utohozi –tani
v. Kuboronga sarufi – wewe anayekuthamini badala ya anayekuthamini wewe

d. **Nafsineni** ni mshauri dhidi ya marafiki wabaya

e. **Toni** ya kushauri/kunasihi/kuliwaza

f. **Lugha nathari**

www.kala.co.ke

ukiwa na rafiki ambaye hukupenda wakati wa mchana. Lakini usiki ukiwadia haonekani. Jua huna rafiki. Huyo sio rafiki . Ni kama mnyama popo

7. a)
Kula nyama kwa wingi na kudhani ni fahari nu kuhatarisha maisha yako
Kula chipsi, kaukau, keki, peremende na vinywaji vya sukari huhatarisha maisha.
Tukipuuza mboaga za majani na za zamani na kutumia za viwandani ni kuhatarisha maisha.
Tukipuuza vyazi vitamu, mihogo na samli ni kuhatarisha maisha
Tunaambukizwa na aina nyingi ya magonjwa kwa sababu ya vyakula vya kisasa/ukengeushi
b)
   i. Urudiaji sauti – o. na a– kuzua wisani/rithimu
   ii. Urudiaji silabi –ni- kutoa mpigo wa sauti rithimu
   iii. Urudiaji neni –mengi, twaliwa - kusistiza ujumbe
   iv. Urudiaji kirai- twaliwa na.. kusistiza ujumbe
c) inkisari – tulapo
utohozi – chipsi,keki
d) Mshauri /mwelekezi
e) Kushauri/kuliwaza/kutahadharisha/kuonya
f) Tukikula kwa wingi chipsi,keki, peremende na kaukau pamoja na vinywaji vya sukari. Na kisha tunaanza kujisifu kwa kusema kuwa ni vitamu katika kinywa. Kwamba vitalize tumbo na kuanza kustarehe vyumbani. Huku macho yetu yametungwa kwa runinga. Jua kuwa tujihadhari wenyewe.
8. a) i) matumizi ya hila/ulaghai kutoka kwa Mutangilu, huwa na funzo, ulaghai kukunduliwa.
ii) Mitindo
Fomula ya utangulizi- hapo zamani
Uhuishi – Mtangilu kupewa sifa za binadamu
Chuku – kubebwa na vijana wane baada ya kushiba
Taswira- kusukuma toroli, Harufu mbaya
Tashbihi – kama radi
Upenyezi – nisaidieni, nataka kujisaidia
Nidaa – salala!
Taharuki – yaliyofuata hayambuliki
Tanakuzi – shilingi kwa ya pili
Mdokezo – mandalina
Takriri- Mandalina, Mandalina.
Kinaya – kula fisi ilhali mila zakataza.
Swali balagha – lakini wapi?
iii. kutambulisha utamaduni
   i. Sherehe za pamoja kama vile arusi
   ii. Kusaidiana vijana kumsukuma Mtangulia
   iii. Mila kukataza kula fisi
   iv. Mila kutokataza kuchuna ngozi
   v. Mandalia kuandalia mumewe chakula
b) Changamoto za kamera

www.kala.co.ke

i. Huhitaji ujuzi
ii. Gharama ya juu kununua
iii. Hitilafu za mitambo zaweza kuathiri
iv. Huhitaji nguvu za umeme
v. Huhitaji fundi /mtaalamu kuzirekebisha
vi. Wahojiwa wengine hubadilisha utendaji wakijua wanarekodiwa
vii. Habari iliyohifadhiwa yaweza kufutika

www.kala.co.ke